
# JICHO LA HAZINA

Msajili Wa Hazina Zanzibar

TOLEO NAMBA 008 SEPTEMBA, 2025


# Pongezi kwa Rais Dk. Mwinyi kwa kuimarisha Mashirika ya Umma



Neema alizozileta Mheshimiwa Rais kupitia mashirika ya umma zimejidhihirisha kwa Kuongezeka kwa mchango wa mashirika ya umma katika pato la taifa









***Mashirika ya umma imara, taifa imara, shiriki katika uchaguzi kwa salama na amani***

# Serikali ya Mapinduzi Zanzibar

# **Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar**

PONGEZI KWA MHESHIMIWA RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI DK. HUSSEIN ALI MWINYI KWA KUIMARISHA MASHIRIKA YA UMMA









**Ofisi ya Majili wa Hazina inatoa wito kwa kila mdau na mwananchi kutoa mapendekezo, ushauri au lolote lile ambaloanahisi litasaidia kulifanya jarida kufikia lengo lake la kuanzishwa na hatimaye kuchangia katika ukusanyaji, usimamizi na matumizi ya fedha katika taasisi za umma. Kwa kushirikiana na kushauriana ndio tutaweza kufanikiwa kujipatia maendeleo tuliyokusudia na kuwa na Zanzibar tunayoitaka.**

# Yaliyomo


**04** SALAMU ZA MSAJILI WA HAZINA ZANZIBAR KWA WENYEVITI NA WATENDAJI WA MASHIRIKA YA UMMA

**05** SALAMU ZA KATIBU MKUU, OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO

**06** PONGEZI KWA MHESHIMIWA RAIS WA ZANZIBAR

**08** UFUATILIAJI WA MIKATABA YA UTENDAJI WA MASHIRIKA YA UMMA

**09** WATENDAJI WA OFISI YA MSAJILI WA HAZINA WAFANYA ZIARA YA MAFUNZO YA KUWAJENGEA UWEZO

**10** OFISI YA MSAJILI WA HAZINA YAFANYA UFUATILIAJI WA MADENI YA GAWIO NA MICHANGO KWA MASHIRIKA YA UMMA NA KUFIKIA MAKUBALIANO

**11** MAJADILIANO YA GAWIO YALETA TIJA NA KUANZA VYEMA KUKUSANYA GAWIO KATIKA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.

**12** OFISI YA MSAJILI WA HAZINA YAFANYA TATHMINI YA MIKATABA WA UTENDAJI YA MWAKA 2024/2025 KWA MARA YA PILI

**13** OFISI YA MSAJILI WA HAZINA YAZINDUWA NYENZO YA KUFANYA UFUATILIAJI (MONITORING TOOLS) NA KUFANYA TATHMINI KWA AJILI YA KUIMARISHA USIMAMIZI WA MIKATABA YA UTENDAJI

# Salamu za Msajili wa Hazina Zanzibar kwa wenyeviti na watendaji wa mashirika ya umma



**NA MWANDISHI WETU**

**Assalamu Alaikum!**

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhaanahu Wataala kwa kutuamsha leo na kutuwezesha kukutana hapa tukiwa na afya njema.

**Ndugu Mgeni Rasmi,**

Napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kukubali kuwa Mgeni Rasmi katika hafla hii adhimu ya kufunga Mikataba ya Utendaji na Taasisi zetu za Uwekekzaji za Umma licha ya kuwa na majukumu mengi na makubwa ya Kiserikali. Napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa wenyeviti wa Bodi pamoja na Wakuu wa Taasisi za Uwekezaji wa Umma kwa kuwa pamoja nasi wakati wa kuandaa Mikatabaa hii na hatimaye kuweza kuhudhuria katika ghafla hii ambayo ni muhimu sana kwa mustakabali wa Taasisi zao na Serikali kwa ujumla.

**Ndugu Mgeni Rasmi,**

Tukio hili ni muendelezo wa kazi za kila siku za Msajili wa Hazina, licha ya kuwa kwako wewe imekuwa mara ya kwanza kuweza kushuhudia uingiaji wa Mikatba ya Utendaji na Taasisi za Uwekezaji wa Umma. Kwani mwaka jana tulifanya isipokua kwa mwaka huu imekuwa na utofauti kwanza kwa kukualika wewe kama mgeni rasmi lakini pili kwa kutoa ripoti ya Tathmini ya Utendaji kazi mbele ya vyombo vya habari. Hivyo, nasema Ahsante kwa kukubali kuwa nasi na Ahsanteni sana nyote kwa kuhudhuria.

**Ndugu Mgeni rasmi,**

Ghafla yetu hii ya leo ambayo tutaishuhudia hivi punde sio tu itaonesha mafanikio ya Ofisi ya Msajili wa Hazina lakini pia itaenda kuonesha na kuchambua kwa undani mafanikio makubwa kwa Taasisi za Uwekezaji wa Umma pamoja na Serikali. Kwani ni dhahiri kwamba utekelezaji wa Sheria hauendi kuonesha kuwa vipi Msajili wa Hazina anafanya kazi lakini unaenda mbali zaidi kwa kwa kuonesha kwa namna gani Taasisi zetu (Mashirika ya Umma) yanafikia malengo ya kuaznishwa kwake.

Kwamantiki hio basi, napenda kuchukua fursa hii kwa kuwashukuru na kuwapongeza Wenyeviti wa Bodi Pamoja wakuu wa Taasisi za Uwekezaji wa Umma na watendaji wote kwa ujumla kwa kufanikisha jambo hili leo kufanyika, kwani najua bila mshikamano huu jambo hili lingekuwa zito kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina pekee. Na kwa upande wa Tathimini ya Mikataba ya kwa mwaka wa fedha 2024/2025 nawashuruku watendaji wa Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kuhakikisha jambo hilo linakamilika kwa wakati na hatimaye limekamilika na leo Ripoti ya Tathmini ya Utendaji inatoka.

**Ndugu Mgeni Rasmi,**

Kwa mujibu wa Sheria hio Kifungu cha 35 kifungu kidogo cha (1) na (2) kinaeleza kuwa "Mwenyekiti na wajumbe wengine wa bodi ya Taasisi ya Uwekezaji ya Umma wataingia katika mikataba ya utendaji kati yao na Msajili wa Hazina kwa mujibu wa vigezo na masharti yalioainishwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina"

Ni kweli kwamba vigezo hivyo vimetolewa katika muongozo na ndio tunaoufuata katika kutimiza masharti haya ya kisheria.

**Ndugu Mgeni Rasmi,**

Pamoja na ufungaji wa Mikataba ya Utendaji kwa mwaka 2025/2026 Ofisi itawasilisha kwa ufupi taarifa ya Tathmini ya Utendaji inayotokana na Mikataba ya Utendaji iliyofungwa mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, taarifa hiyo inaakisi uchambuzi wa kina wa utendaji wa taasisi hizi, taasisi ambazo ni nguzo kuu za uchumi wetu, watoa huduma muhimu kwa umma na vyanzo vikuu vya ajira kwa wananchi.

Hata hivyo, taarifa hii inatoa uelewa muhimu na mapendekezo ya kimkakati, yanayolenga kuimarisha usimamizi wa rasilimali watu, kuendeleza utawala bora, kuboresha uwezo wa ufanisi, na kuhakikisha uendelevu wa muda mrefu wa taasisi hizi muhimu. Nitumie fursa hii kusisitiza kwamba tathmini hii si zoezi la uwajibikaji pekee, bali ni dhamira ya dhati ya uwazi na uadilifu wa takwimu. Tathmini zote zimefanywa kwa kufuata viwango vilivyowekwa, bila migongano ya maslahi, na kwa kutumia takwimu sahihi na zinazoaminika kutoka Taasisi zenye za Uwekekzaji wa Umma.

**Ndugu Mgeni Rasmi,**

Mwisho, napenda kuchukua nafasi hii kuendelea kukushukuru wewe Mgeni Rasmi kuja kuungana nasi ili kutupatia nasaha zako na hatimaye kushuhudia uingiaji wa Mitataba ya Utendaji kwa Taasisi za Uwekezaji wa Umma kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Sisi Ofisi ya Msajili wa Hazina tunaema "Mashirika ya Umma imara, taifa imara, shiriki katika uchaguzi kwa salama na amani"

# Salamu za Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dkt. Juma Malik Akil kwa Wenyeviti wa Bodi wa Mashirika ya Umma

**NA MWANDISHI WETU**

Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehma kwa kutujalia afya njema tukaweza kujumuika hapa siku ya leo.

Nimshukuru sana Msajili wa Hazina Zanzibar pamoja na Wenyeviti wa Bodi kwa kunialika ili niwe Mgeni Rasmi wa tukio hili muhimu la ufungaji wa Mikataba ya Utendaji kwa Taasisi zenu kwa



mwaka 2025/2026. Ufungaji wa Mikataba ya Utendaji upo kwa mujibu wa Sheria ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma Nam. 6 ya mwaka 2021 chini ya kifungu cha 35.

Hivyo, heshima sana kwangu na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango pamoja na Afisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji. Utaratibu huu unaoendelea kufanyika kila ni mzuri kwani mbali ya kutekeleza masharti ya Sheria bali pia unaimarisha ufanisi wa Taasisi zetu wa Uwekazaji wa Umma. Lakini kwa mwaka huu tukio hili limekuwa la kipekee kwa kuhudhuriwa na Makatibu wakuu wa Wizara kuu zinazoshughulikia masuala mazima ya Fedha,Mipango, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ikizingatiwa kwamba nguzo kuu za uchumi wetu pia unatokana na uwekezaji uliofanywa katika Taasisi hizi (Mashirika ya Umma).

Niendelee kumpongeza sana Msajili wa Hazina kwa kushirikiana na Wakuu wa Taasisi za Uwekezaji wa Umma (Mashirika ya Umma) kwa kutekeleza takwa hili la kisheria la ufungaji wa Mikataba ya Utendaji. Aidha, nimefurahika kusikia kwamba mwaka jana tuliweza kuingia mikataba hiyo na tayari Tathmini ya Utendaji wa Mikataba hiyo imeshafanyika kwa kushirikiana na Taasisi zenyewe na taarifa zake zitawasilishwa mbele yetu hii kwa ajili ya kuzingatia yaliyonekana ili katika mwaka huu wa 2025/2026 tupate kuboresha zaidi kasoro zilizojitokeza.

**Ndugu Wenyeviti wa Bodi**

Nina imani ni kuwa ufangaji wa Mikataba ya Utendaji utachochea na kuendeleza utendaji kazi na mashirikiano kwa maendeleo ya taasisi zetu na kuimarisha dhamira yetu endelevu ya uwazi, uwajibikaji na uimarishaji wa ufanisi wa kiutendaji katika taasisi za uwekezaji wa umma.

Ni wazi kwamba Tathmini ya utendaji itakayowasilishwa inatokana na Mikataba ya Utendaji iliyosainiwa baina ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Taasisi za Uwekezaji wa Umma, kupitia Bodi zenu husika kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Hivyo Mikataba hii siyo tu ni nyenzo za kiutawala, bali pia ni nyenzo ya kimkakati inayoendana na juhudi pana za Serikali za kuimarisha utawala bora, nidhamu ya matumizi ya fedha na utoaji wa huduma bora katika mashirika yetu ya umma.

Kama tunavyofahamu kwamba malengo ya tathmini ni kuangalia kwa kiwango gani taasisi hizi zimetimiza malengo ya utendaji mliyokubaliana, kwa kutumia Viashiria Muhimu vya Utendaji (Key Performance Indicators – KPIs) vilivyobainishwa kwa uwazi wakati wa kufunga Mikataba.

**Ndugu Wenyeviti wa Bodi**

Nimeelezwa kwamba viashiria vilivyotumika katika Tathmini iliyofanywa na kufikia matokeo ya kiutendaji vilikua ni:

- Usimamizi wa Rasilimali Watu;
- Utawala Bora na Udhibiti wa Ndani;
- Huduma kwa Wateja;
- Utekelezaji wa Majukumu ya Msingi ya Taasisi; na
- Usimamizi wa Rasilimali Fedha.

Pia nimeelezwa kwamba mbinu zilizotumiwa katika Tathmini hiyo ilikuwa ni Uchambuzi wa nyaraka, Uchambuzi wa takwimu za kifedha na utendaji, Mahojiano na wadau muhimu pamoja na Ziara za ukaguzi katika baadhi ya Taasisi za Uwekezaji wa Umma.

Ni matumaini yangu kwamba tathimni hiyo ilifanyika kwa uwazi na matekeo yaliyoainishwa katika Taarifa iliyochapishwa katika kitabu ni sahihi na itaweza kutumika kwa ajili ya kuimarisha utendaji kazi wa Mashirika yetu pamoja na wengine kuweza kusoma walipokosea kujisahihisha.

**Ndugu Wenyeviti wa Bodi**

Tunatarajia kwamba Mikataba hii itakayoingiwa leo hii itasaidia kuwajengea uwezo nyinyi binafsi ili kuimarisha utendaji kazi na utoaji wa huduma bora kwa taasisi zenu pamoja na wanachi kwa ujumla. Aidha, Katika nyakati hizi, ni muhimu kwa Wenyeviti wa Bodi na wakuu wa taasisi kubaini changamoto zinazoikabili taasisi zao, watendaji wao, jamii na miradi ambayo inatekelezwa ili Serikali iweze kuchukua hatua stahiki kwa wakati.

Na ni wazi kwamba katika kila kazi hakukosi changamoto ambapo kama taasisi tunatakiwa kuzifanya kuwa fursa pamoja na mapendekezo yatakayotolewa na Ofisi ya Msajili wa Hazina kuweza kuyafanyia kazi kwa ajili ya kuimarisha taasisi zetu na kuimarisha uchumi wa nchi,na kuwapatia huduma bora wananchi wa Zanzibar.

Kama tunavyoelewa kwamba mnamo tarehe 29 Oktoba,2025 nchi yetu itakua na Uchaguzi Mkuu wa Serikali hivyo tunaunga mkono kauli ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi ya kudumisha Usalama na Amani kabla, wakati na baada ya uchaguzi kwani kuna maisha baada ya uchaguzi."



# PONGEZI KWA MHESHIMIWA RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA KUIMARISHA MASHIRIKA YA UMMA

MASHIRIKA ya umma ni mhimili muhimu wa uchumi na maendeleo ya kijamii nchini. Ni injini zinazochochea ukuaji wa biashara, ajira, mapato ya Serikali na utoaji wa huduma kwa wananchi. Katika kipindi cha uongozi wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi mashirika ya umma yamepata neema kubwa kupitia mageuzi, sera makini na maono ya kimaendeleo.

**Utawala Bora na Uwajibikaji:** Kupitia mikataba ya kiutendaji na mikataba ya ulipaji wa gawio, mashirika yamewekewa vigezo vya wazi vya kupimika.

**Kuimarisha Uchumi:** Mashirika yamechangia mapato makubwa Serikalini kupitia gawio, hivyo kusaidia utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Huduma kwa Wananchi:** Huduma zimeboreshwa, zikijumuisha upatikanaji wa bidhaa, huduma za kifedha, hifadhi ya jamii na mawasiliano.

**Uwekezaji wa Kimkakati:** Mashirika yamepewa fursa ya kupanua wigo wa uwekezaji katika maeneo yenye faida kubwa kwa taifa.

**Neema za Dr Mwinyi kwa Mashirika**

Neema alizozileta Mheshimiwa Rais kupitia mashirika ya umma zimejidhihirisha kwa Kuongezeka kwa mchango wa mashirika ya umma katika pato la taifa, Uimarishaji wa huduma za kijamii kama afya, hifadhi ya jamii na usafiri wa majini na anga, Kuimarisha nafasi ya Zanzibar katika soko la kikanda na kimataifa kupitia mashirika ya biashara na bandari na Kuibua fursa za ajira kwa vijana na kuongeza usalama wa ajira kwa wananchi.

**Mashirika ya Uwekezaji wa Umma yamegawanywa katika Fursa Muhimu za Uwekezaji kwa Sekta na Taasisi ikiwemo:**

1. Miundombinu na Makaazi (ZHC, ZPC, ZAA)
2. Nishati na Huduma (ZECO, ZAWA)
3. Kilimo, Uvuvi na Usindikaji (ZSTC, ZAFICO, ZASCO)
4. Huduma za Kidigitali na Vyombo vya Habari (ZICTIA, ZMUX, ZBC);
5. Huduma za Kifedha na Bima (PBZ, ZIC, ZSSF);
6. Huduma za Afya na Kijamii (ZHSF, ZSSF); na
7. Huduma za Bandari na Usafiri Baharini (SHIPCO, ZPC)

**Mafanikio ya Mashirika ya Uwekezaji ya Umma**

**Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC):**

Uimarishaji wa miundombinu ya bandari, kupanua huduma za usafirishaji na kuongeza mapato Serikalini kupitia ulipaji wa gawio. Uingiaji wa mkataba na kampuni ya kimataifa kutoka Ufaransa (AGL/ ZMT) kuendesha Bandari ya Malindi. Uboreshaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Bandari (E-PORT),Uwekezaji wa dhana za kutoa huduma Bandari. Ujenzi wa Bandari Mpya na Maendeleo ya Miundombinu katika eneo la Malindi Unguja - Shumba Pemba na Ujenzi wa miundombinu ya CBM (Ushughulikiaji wa Mizigo/ Mabaki) na Hifadhi ya Mikakati ya Mafuta na Gesi na Ugawaji unaoendelea wa vitalu vya mafuta na gesi katika Mangapwani.

**Shirika la Meli Zanzibar (SHIPCO)**

Serikali imeanza ujenzi wa Boti mbili (2) za kasi kubwa na inaendelea kufanya marekebisho kwenye meli ya MV Mapinduzi II, ambapo marekebisho yamefika kukamilika.

**Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC)**

ZHC kupitia dira yake inaitaka ***"Kuwa taasisi inayoongoza katika sekta ya biashara ya Mali isiyohamishika Zanzibar" na dhamira yake ni "Kuwa kituo cha ubora katika utoaji wa makazi ya ubora na yanayoweza kumudu kuwapatia watu wa Zanzibar".***

Katika kutimiza hili, Shirika limeweza kujenga nyumba 92 za makazi, zikiwa 84 huko Unguja na 8 huko Pemba. Aidha, ili kuimarisha makazi salama na ya ubora kwa wananchi, Shirika limeanza maandalizi na utekelezaji wa ujenzi wa nyumba 1,117 huko Unguja, ikiwa ni pamoja na Mradi wa New Chumbuni na nyumba 180 kwenye Kisiwa cha Pemba. Vivyo hivyo, Shirika limefanya matengenezo kwenye nyumba kadhaa za makazi za wananchi, ikiwa ni pamoja na zile zilizopo Michenzani.

**Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ):**

PBZ imeongeza umarishaji wa kifedha, uwajibikaji, upatikanaji wa mikopo kwa wananchi na wafanyabiashara, huduma bora zinazotolewa na kuimarisha nafasi ya Zanzibar katika huduma za kifedha za kikanda. Gawio limeongezeka kutoka TZS 7 bilioni hadi kufikia TZS 10 bilioni sawa na ongezeko la asimilia 42.85 ya gawio lililokusanywa mwaka 2023. Kuimarika kwa ufunguzi wa matawi mepya ya Benki ikiwemo Arusha.

**Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF):**

Uboreshaji wa huduma za hifadhi ya jamii umewawezesha wananchi kupata mafao kwa ufanisi na kuimarisha hifadhi ya kijamii. Shirika limeanzisha na inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, ikijumuisha Mradi wa Soko la Mombasa na mradi wa nyumba za makazi katika Jiji la Dk. Hussein Mwinyi, ukiwa na uwekezaji wa jumla unaotarajiwa wa TZS bilioni 37.8.

Miradi iliyokamilika ni pamoja na Mradi wa eneo la Maegesho ya Magari Malindi, Stendi ya Magari ya Kijangwani na eneo la Biashara na Michezo Mbweni ambapo jumla ya TZS 16.3 Bilioni zilitumika.

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii yaingia Mkataba wa Uendeshaji wa Mabasi ya abiria yanayotumia Umeme na Kampuni ya GRT Investment LL.CFZ.

**Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC):**

Kuongeza thamani ya mazao ya kilimo hususan karafuu, likiwapa wakulima masoko bora na kipato cha uhakika. Uanzishaji wa Mfumo Mpya wa Mnada Mtandaoni, Uanzishwaji wa Mfumo wa Ununuzi wa Karafuu, Uimarishaji wa zao la karafuu. ZSTC inaendelea na juhudi zake za kuwapatia miche ya mikarafuu Wakulima pamoja na nyezo za kuatikia miche hio.

***Kuanzisha Mfumo mpya wa Online Auction***

ZSTC imefanikiwa kuandaa mfumo wa mnada wa karafuu unaojulikana kama "Online Auction" na kusajili minada miwili iliyosimamiwa na Shirika; Mfumo huu umeimarisha uwazi na ufanisi katika uuzaji wa karafuu; Mfumo umechangia kuweza kupata kigezo (benchmark) kizuri cha bei ya karafuu;na Umesaidia kuongeza mapato kwa Shirika kupitia ada ya usajili (commitment fee).

***Kuanzisha Mfumo wa Kununulia Karafuu***

Mfumo wa kidijitali kwa ununuzi wa karafuu umeanzishwa na kutumika katika Vituo vya ununuzi wa karafuu;

Mfumo huo umeunganishwa na programu tumizi ya kiganjani (mobile app) ambayo inarahisisha upatikanaji wa taarifa na usimamizi wa shughuli za ununuzi papo kwa papo (real time).

**Mafanikio yaliyopatikana na ZSTC**

a) Kuanza kuitumia bandari ya Mkoani Pemba kwa kusafirishia karafuu nje ya nchi;

b) kuongeza bidhaa mpya aina ya ZanGarlic Paste na Bitter Orange Oil;

c) Kufunga Vyungu vipya 2 vya uzalishaji wa mafuta ya Mimea;

d) Kuanzisha Mfumo ya "Online Auction" na Mfumo wa Kununulia Karafuu vituoni (smart buying);

e) Kuanzisha mfumo wa Mikataba baina ya MD na Watendaji;

f) Kupata alama ya ubora ya ZBS kwa bidhaa za ZSTC.

**Shirika la Bima Zanzibar (ZIC):**

Kupanua huduma zake za bima na kuhakikisha wananchi na mali zao wanakuwa salama dhidi ya majanga.zikiwemo huduma ya ZIC Takaful, Kuazishwa Sera ya Bima ya lazima kwa wageni wote wanaofika Zanzibar (Inbound Travel Insurance) yenye lengo la kutoa kinga dhidi ya majanga na dharura pindi yakitokea ndani ya siku tisini na mbili (92) popote pale Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Shirika limeweza kuongeza Mapato yatokanayo na ada za Bima kutoka TZS 19 billioni kwa kipindi cha mwaka 2020 hadi TZS 130.74 billioni katika mwaka 2024). Ongezeko hili ni kutokana na kuongezeka kwa uaminifu wa Wananchi katika kutumia bidhaa za Bima na upanuzi wa huduma za Bima katika kuwakinga na majanga mbalimbali ambayo yanaweza kuwatokea.

Kutanua na kuongeza wigo wa biashara ya Bima kwa mashirikiano ya kimkakati na Makampuni na Mabenki mbalimbali katika mfumo wa benkibima kama vile Shirika la Posta Tanzania, NMB Bank, CRDB Bank, EXIM Bank, TCB Bank, PBZ Bank, Benki ya Africa, Mwalim Commercial Bank, Mucoba Commercial Bank na FAIDIKA/ LETSHGO) kwa Lengo ka kuongeza mapato ya Shirika.

**Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC):**

Limeboresha vifaa na vipindi vyake, hivyo kuwa chombo kikuu cha mawasiliano, elimu na burudani kwa wananchi.

**Pongezi na Shukrani**

Kwa niaba ya mashirika ya umma Zanzibar, tunampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa maono yake ya kijasiri, uongozi wa hekima na dhamira yake thabiti ya kuyawezesha mashirika ya umma kuwa injini ya maendeleo.Uongozi wake umeleta mabadiliko chanya yanayoshuhudiwa na kila mmoja, na umeweka msingi imara wa uwajibikaji, tija na ufanisi katika taasisi za umma.

Mashirika ya umma Zanzibar leo yanasimama imara, yakichangia mapato ya Serikali, kutoa huduma bora kwa wananchi na kushiriki kikamilifu katika kukuza uchumi wa taifa. Haya yote ni matunda ya uongozi wa busara wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Rais ameweka msingi imara wa mashirika ya umma Zanzibar – msingi unaojikita katika uwajibikaji, huduma bora na tija kwa taifa. Neema aliyoiweka imejidhihirisha kwa wananchi na vizazi vijavyo vitafaidika na matunda haya.

Kuanzishwa kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar imepelekea Ofisi hiyo kuwa na Mamlaka zaidi ya kiutendaji na usimamizi (Regulator) kuchunguza, kukagua utendaji wa Taasisi za Uwekezaji wa Umma na Usimamizi wa Mali za Umma hapa Zanzibar ili kuweza kwenda sambamba na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar "Zanzibar Vision 2050" na Ilani ya Chama cha Mapinduzi "CCM Manifesto".

# UFUATILIAJI WA MIKATABA YA UTENDAJI WA MASHIRIKA YA UMMA

Ofisi ya Msajili wa Hazina, kwa mujibu wa Sheria Na. 6 ya mwaka 2021, imeendelea kusimamia mashirika na taasisi za umma ili kuhakikisha yanaendana na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 ambapo Ofisi ilifanya ufuatiliaji wa ripoti za utekelezaji wa mikataba ya kiutendaji kwa mashirika ya umma Zanzibar ambapo viashiria Muhimu vya Mikataba ya Utendaji Kazi vilitumika.

Aidha, malengo ya tathmini ni kuangalia kwa kiwango gani taasisi hizi zimetimiza malengo ya utendaji mliyokubaliana, kwa kutumia Viashiria Muhimu vya Utendaji (Key Performance Indicators – KPIs) vilivyobainishwa kwa uwazi wakati wa kufunga Mikataba.

Katika ufuatiliaji wa Mikataba hiyo viashiria vitano (5) muhimu huangaliwa kwa njia ukaguzi na kuthibitisha taarifa zake kwa kila shirika viashiria vilivyotumika katika tathmini iliyofanywa na kufikia matokeo ya kiutendaji vilikua Usimamizi wa Rasilimali Watu (People Management);Utawala Bora na Udhibiti wa Ndani (Good Governance and control); Huduma kwa Wateja (Customer Service); Utekelezaji wa Majukumu ya Msingi ya Taasisi (Core Functions of Institution Mandates); na Usimamizi wa Rasilimali Fedha (Financial Stewardship).

Mikataba hii siyo tu ni nyenzo za kiutawala, bali pia ni nyenzo ya kimkakati inayoendana na juhudi pana za Serikali za kuimarisha utawala bora, nidhamu ya matumizi ya fedha na utoaji wa huduma bora katika mashirika yetu ya umma.

Jumla ya Mashirika ambayo yaliingia mikataba wa Utendaji kazi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yalikua kumi na Moja (11) likiwemo ZHSF, ZSSF, ZSTC, ZAA, ZIC, ZBC, ZPC, CGN, ZPDC, ZICTIA, na SHIPCO. Aidha, Mafunzo ya Vitendo yaliweza kufanyika kwa Shirika la ZHSF, ZSSF, ZBC, ZPC, ZIC, ZSTC, ZAA pamoja na SHIPCO kwa kuingiza taarifa zao katika nyenzo.



*Watendaji wa Idara ya Mitaji ya Umma na Uwekezaji wafanya ufuatiliaji wa kufanya ufuatiliaji wa kuimarisha Mikataba ya Kiutendaji katika Benki ya Watu wa Zanzibar PBZ Mipirani.*



*Afisa Mitaji ya Umma Ndugu Abdullah Salum Abdullah akitoa ufafanuzi wa jinsi ya upigaji wa hesabu katika Nyenzo ya kufanya ufuatiliaji wa Mashirika ya Uwekezaji wa Umma.*

# WATENDAJI WA OFISI YA MSAJILI WA HAZINA WAFANYA ZIARA YA MAFUNZO YA KUWAJENGEA UWEZO

LENGO kuu la utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ni Kuimarisha usimamizi wa mali za umma na mashirika ya umma ambapo Programu kuu ya uimarishaji huo ni Usimamizi wa Mali za Umma na Uwekezaji wa Mashirika ya Umma. Katika Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2025/2026 Idara ya Mitaji ya Umma na Uwekezaji iliandaa shughuli ya kufanya ziara za kikazi katika Ofisi ya Msajili Tanzania Bara kwa ajili ya kubadilishana uzoefu.

Katika Robo mwaka ya mwaka 2025/2026 jumla ya watendaji watano (5) walishiriki ziara ya mafunzo ya siku 5 katika Ofisi ya Msajili wa Hazina Tanzania Bara. Ziara hii ililenga kujenga uwezo katika usimamizi wa taasisi za uwekezaji za umma, hasa kwenye maeneo ya Uchambuzi wa Bajeti (Budget Scrutinization), Tathmini ya Bodi za Taasisi (Board Evaluation), Ukusanyaji wa Gawio na Michango na Uandaaji wa Sera za Gawio suala ambalo limepelekea kuimarisha uwezo wa kiufundi katika kuchambua bajeti za taasisi za umma, Kuelewa mchakato wa ukusanyaji wa mapato na gawio, Kujifunza utawala bora kupitia tathmini za utendaji kazi wa kurugenzi za Bodi na Kuongeza ushirikiano na uzoefu wa pamoja kati ya Zanzibar na Tanzania Bara.

Kupitia ziara hiyo watendaji hao waliweza kujifunza Tathmini ya Wajumbe wa Bodi ambapo tathmini hiyo hufanyika kila mwaka kwa lengo la kupima ufanisi wa uongozi ambapo huhusisha Bodi kwa ujumla, kamati, mwenyekiti, wajumbe mmoja mmoja na katibu. Uchambuzi wa Bajeti, ambapo mazingatio ya Bajeti za Mashirika ni lazima izingatie mpango mkakati, MTEF, na uwiano wa fedha za maendeleo ambapo Taasisi huwasilisha bajeti miezi 3 kabla ya mwaka wa fedha kuisha baada ya marekebisho, bajeti huidhinishwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Mapato ya Hazina, Vyanzo vikuu vya uchangiaji wa Mapato ya Serikali ni ulipaji wa asilimia 15 ya mapato ghafi, gawio, surplus, CSR, riba za mikopo, makato ya TCRA. kwa upande uimarishaji wa ukusanyaji wa mapato njia zinazotumika kuongeza mapato hayo ni pamoja na matumizi ya mifumo ya kidigitali, usimamizi madhubuti, ongezeko la uwekezaji na mashirikiano ya kitaasisi.

Aidha,kwa upande wa watendaji na Ofisi kwa ujumla ziara hii imeweza kuongeza uelewa na uwezo wa kitaalamu kwa watendaji katika kusimamia taasisi za uwekezaji za umma ambapo kupitia mafunzo haya, ufanisi wa ukusanyaji mapato, uchambuzi wa bajeti, na tathmini ya bodi unatarajiwa kuimarika. Halikadhalika, uimarishaji wa ushirikiano wa Ofisi ya Msajili wa Hazina Tanzania Bara na Zanzibar unandelea kuwa nguzo ya mafanikio, uimarishaji wa ya utawala bora na uwajibikaji wa kifedha.

# OFISI YA MSAJILI WA HAZINA YAFANYA UFUATILIAJI WA MADENI YA GAWIO NA MICHANGO KWA MASHIRIKA YA UMMA NA KUFIKIA MAKUBALIANO



***Mkuu wa Idara ya Mitaji ya Umma na Uwekezaji Ofisi ya Msajili wa Hazina Ndugu Ramia Mohammed Ramia (kwanza kushoto) afanya mazungumzo ya ulipaji wa Gawio la Serikali Mkurugenzi Mkuu wa ZICTIA Enginner Shukuru Suleiman Awadh (kwanza kulia) akifuatilia hoja zilizowasilishwa za ulipaji wa Mchango wa Serikali***


OFISI ya Msajili wa Hazina imeendesha mchakato wa ufuatiliaji wa ulipaji wa gawio na michango kwa Taasisi za Uwekezaji wa Umma ambapo jumla ya Mashirika manane (8) ya Uwekezaji wa Umma yanayostahili kulipa mchango na gawio yamefuatiliwa na kushiriki katika vikao vya kujadili ulipaji wa gawio (ZECO, ZHC, PBZ, ZIC, ZPC, ZSTC, SHIPCO, ZICTIA)

Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imeweza kuipangia Ofisi ya Msajili wa Hazina jumla ya TZS 25 Bilioni kama lengo la ukusanyaji wa Mapato yasiyokua ya Kodi. Katika jitihada za kuona kwamba Mapato hayo yanawasilishwa Serikalini,Ofisi ya Msajili wa Hazina iliandaa vikao kazi vya kujadili ulipaji wa gawio na kufikia makubaliano ya pamoja ya namna bora ya uwasilishaji wa gawio kwa mwaka mpya wa fedha huku ikijumuisha na madeni ya nyuma ambapo hadi kufikia mwezi Juni,2026 jumla ya TZS 24 Bilioni zitakusanywa.

Kwa mujibu wa utaratibu, kiwango cha ulipaji gawio kwa sasa ni asilimia 50 ya faida baada ya kutoa kodi za Serikali ambapo utaratibu uliopendekezwa wa kulipa ni kuimarisha utaratibu wa malipo ya kila mwezi (badala ya kusubiri baada ya kufunga hesabu, kuanzisha ratiba ya malipo ya robo mwaka kwa taasisi zenye mapato yasiyo thabiti (mfano ZSTC), kuongeza usimamizi na ukaribu kati ya Msajili wa Hazina na mashirika kwa kuweka maafisa kiunganishi, Kuimarisha uwazi wa hesabu na ripoti kwa kushirikisha CAG mapema, na kutafuta mbinu za ubunifu wa fedha (financial restructuring) ili mashirika yenye madeni makubwa (mfano SHIPCO, ZECO) yaweze kulipa bila kudhoofisha uendeshaji wa Mashirika hayo.

Aidha,katika hatua za awali Ofisi ya Msajili wa Hazina imefunga mkataba wa ulipaji wa gawio na jumla ya Mashirika manne (4) ambapo mashirika yanye ni Pamoja na SHIPCO, ZSTC, ZIC na ZPC. Serikali,kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina itaendelea kufuatilia na kusimamia kwa ukaribu mashirika ya umma na uwekezaji wake ili kuhakikisha rasilimali za taifa zinawanufaisha wananchi kwa kuchochea ukuaji wa uchumi, kuongeza mapato ya serikali na kuboresha ustawi wa kijamii.

*Mheshimiwa Dr. Saada Mkuya Salum akabidhiwa mfano wa Hundi ya gawio la Serikali kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya PBZ Ndugu Joseph Abdalla Meza na Mkurugenzi Mwendeshaji wa PBZ Ndugu Fahad S. Hamid.*




# MAJADILIANO YA GAWIO YALETA TIJA NA KUANZA VYEMA KUKUSANYA GAWIO KATIKA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.

Ofisi ya Msajili wa Hazina imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kuhakikisha mashirika ya uwekezaji wa umma yanachangia kwenye mapato ya Serikali kupitia gawio.

Katika hatua za ulipaji wa gawio la Serikali, majadiliano ya ulipaji wa gawio yameanza kuleta manufaa kwa mashirika kuanza kutoa Gawio la mfano katika miezi ya mwanzo ya utekelezaji wa makubaliano sambamba na Mashirika ambayo hayajawahi kutoa gawio kuanza kutoa Gawio ambapo Shirika la Bandari limeendeleza ulipaji wa Gawio la kila mwezi kwa kuwasilisha **TZS 600 million**, Shirika la Meli Zanzibar (SHIPCO) kwa mara ya kwanza limeanza kutoa gawio la Serikali ambapo jumla ya **TZS 200 million** zimewasilishwa**.** Aidha, Shirika la Bima la Taifa limewasilisha jumla ya **TZS 280 million**, Pamoja na Shirika la Nyumba la Zanzibar limetoa TZS **50** million, na kufanya jumla ya makusanyo kufikia TZS **1.130 billion.**

Kwa kipekee itakumbukwa kwamba mnamo tarehe 25 Agosti,2025 Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) iliweza kukabidhi mfano wa hundi yenye jumla ya **TZS 10 bilioni** katika mkutano mkuu wa wanahisa kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Mipango Dr.Saada Mkuya Salum na kuweza kuvunja rikodi ya Shirika lililolipa gawio ya kima kikubwa tokea kuanzishwa kwa Mashirika ya Uwekezaji ya Umma Zanzibar.

**Malipo ya Gawio tangia kuanzishwa kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar.**

| MWAKA | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | Jumla ( Bilioni) |
|---|---|---|---|---|
| JUMLA | 13,705 | 550 | 8,510 | 22,765 |

Aidha ikilinganishwa gawio lililokusanywa katika kipindi cha Julai na Agosti,2025/2026 na kipindi cha mwaka jana jumla ya TZS 1.13 bilioni zimekusanywa ukitoa TZS 7 bilioni iliyowasilishwa na PBZ mwaka jana.

Matarajio ya ukusanyaji wa gawio katika mwaka wa fedha 2025/2026 ni kukusanya gawio ambalo halijawahi kukusanywa ukitoa jumla ya TZS 13.7 bilioni zilizokusanywa mwaka wa fedha 2022/2023. Mafanikio ni kiwango cha makusanyo ya gawio tangu kuanzishwa kwa mfumo huu, unaongeza uimarishaji na uwajibikaji wa mashirika ya umma katika kutekeleza makubaliano na kuonesha nidhamu ya na utekelezaji wa majukumu.

Aidha, Ofisi itaendelea kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa makubaliano ya gawio, kuongeza hamasa na msukumo kwa mashirika mengine kufuata utaratibu ulioanzishwa.

Makusanyo ya gawio kwa mwaka huu yanaonyesha mafanikio makubwa ya Ofisi ya Msajili wa Hazina katika kuimarika mwaka hadi mwaka kwenye ukusanyaji wa mapato. Hatua hii ni chachu ya kuongeza mchango wa mashirika ya umma katika ustawi wa uchumi wa Zanzibar na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2050.

*Mkuu wa Idara ya Mitaji ya Umma na Uwekezaji Ofisi ya Msajili wa Hazina Ndugu Ramia Mohammed Ramia (kwanza kushoto) afanya mazungumzo ya ulipaji wa Gawio la Serikali na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Bima Ndugu Jape U. Khamis (watatu kulia) Makao Mkuu ya Ofisi ya Msajili wa Hazina, Zanzibar.*



 MASHIRIKA YA UMMA IMARA, TAIFA IMARA, SHIRIKI KATIKA UCHAGUZI KWA SALAMA NA AMANI


# OFISI YA MSAJILI WA HAZINA YAFANYA TATHMINI YA MIKATABA WA UTENDAJI YA MWAKA 2024/2025 KWA MARA YA PILI

KATIKA Kuimarisha Ufanisi na Uwajibikaji wa Taasisi za Uwekezaji wa Umma Zanzibar, Ofisi ya Msajili wa Hazina imekamilisha tathmini ya mwaka ya utekelezaji wa mikataba ya utendaji kwa Taasisi za Uwekezaji wa Umma (PIEs) kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Tathmini hii, ni sehemu ya utekelezaji wa Sheria Na. 6 ya 2021 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma, inalenga kuhakikisha taasisi hizi zinafanya kazi kwa uwazi, ufanisi na kuzingatia viwango vya utawala bora.


**Matokeo ya Tathmini**

Tathmini ilibaini kuwa taasisi nyingi zimeonesha juhudi za kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, ambapo taasisi kama Zanzibar Social Security Fund (ZSSF), Zanzibar Communication Corporation (ZICTIA), Shirika la Magazeti ya Serikali (CGN) na Zanzibar Airports Authority (ZAA) zimepata alama ya Bora (Excellent) katika maeneo mbalimbali. Hata hivyo, changamoto kubwa zilizobainishwa ni, kukosekana kwa tathmini za kina za hatari (Risk Assessment), Ukosefu wa mpango wa mwendelezo wa kazi (Business Continuity Plan - BCP) katika taasisi nyingi, Ucheleweshaji katika kufanya ukaguzi wa ndani na wa kisheria.

**Matokeo ya Jumla ya Tathmini**




**Ulinganishi wa Uchambuzi wa Utendaji kazi wa Taasisi za Uwekezaji wa Umma.**




Tathmini ya alama za utendaji wa wastani kwa taasisi za Uwekezaji wa Umma inaonyesha nguvu kubwa katika utawala bora na udhibiti wa ndani lakini udhaifu katika usimamizi wa rasilimali fedha.

Utawala Bora na Udhibiti wa Ndani umekuwa na kiwango cha juu zaidi cha 84.7%, ukifuatwa na utekelezaji wa majukumu ya msingi za taasisi ambazo ni wajibu kwa 74.8% na Huduma kwa Wateja kwa 73.6%. Alama za chini zaidi ni Usimamizi wa Rasilimali watu (68.08%); na Usimamizi wa Rasilimali Fedha ikiwa na alama ya chini kwa 67.36%. Kudumisha utawala ubora wakati wa kuboresha usimamizi wa wafanyakazi na umarishaji wa huduma za kifedha ni muhimu.

**Mapendekezo**

Kwa kuzingatia matokeo ya tathimini iliyofanyika, Ofisi ya Msajili wa Hazina imependekeza hatua zifuatazo kuchukuliwa Taasisi zote za Uwekezaji wa Umma zifanye tathmini ya hatari na kuandaa rejesta ya hatari ili kusimamia changamoto zinazoweza kuathiri huduma, Kuanzishwa na kusimamiwa kwa mpango wa mwendelezo wa kazi ili kuhakikisha huduma muhimu haziathiriki endapo changamoto zitajitokeza na Kufanyika kwa ukaguzi wa ndani kwa wakati na utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi ili kuimarisha uwajibikaji wa kifedha. Utolewaji wa mrejesho wa utendaji kazi kwa wafanyakazi mara kwa mara kwa lengo la kudhibiti utendaji kazi wa wafanyakazi, kukusanya na kuandika (kuweka rekodi) ya malalamiko ya wafanyakazi, maelezo ya mafunzo, malalamiko ya wateja na masuala yanayohusiana ili kuboresha ustawi wa wafanyakazi na wateja.

Taasisi za Uwekezaji wa Umma ndizo injini za maendeleo ya Zanzibar ambapo taasisi hizo zinatoa ajira, huduma muhimu kwa wananchi, na kuchangia katika mapato ya Serikali (Kodi na Gawio). Kwa tathmini hii, wananchi wanapata uhakika kuwa rasilimali za umma zinatumika kwa tija na uwazi.

Aidha, Ofisi ya Msajili wa Hazina itaendelea kusimamia kwa karibu mikataba ya utendaji kazi, kuhakikisha kuwa taasisi zote za umma zinafanya kazi kwa kuzingatia viwango bora vya utawala, ufanisi na uadilifu. Lengo kuu ni kulinda maslahi ya wananchi na kuendeleza maendeleo endelevu ya Zanzibar.

# OFISI YA MSAJILI WA HAZINA YAZINDUWA NYENZO YA KUFANYA UFUATILIAJI (MONITORING TOOLS) NA KUFANYA TATHMINI KWA AJILI YA KUIMARISHA USIMAMIZI WA MIKATABA YA UTENDAJI



***Watendaji wa Idara ya Mitaji ya Umma na Uwekezaji Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar katika mataarisho ya Nyenzo ya kufanya ufuatiliaji wa Mashirika ya Uwekezaji wa umma (monitoring tools) na kufanya tathmini kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa mikataba ya utendaji.***

Ofisi ya Msajili wa Hazina imeweza kuzinduwa nyenzo 2 kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji (Monitoring Tools) na kufanya tathmini ya Utendaji kazi (Performance Contract Evaluation Tool) katika mikataba ya kiutendaji ambapo nyenzo hizo zimeanza kutumika kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa mikataba ya kiutendaji ambapo nyenzo hizo zitarahisisha upatikanaji wa taarifa kwa Mashirika ya umma, kuzihifadhi na kuweza kusaidia katika kufanya tathmini kwa urahisi zaidi kuliko kutumia "manual Monitoring Tool".

Nyenzo hiyo imesanifiwa kwa kutumia programu ya Jedweli ya Excel, ikiruhusu uingizaji kwa taarifa, uchambuzi wa robo mwaka na wa mwaka mzima, na kubaini mwenendo wa mashirika.

Aidha, nyenzo hii ni sehemu ya jitihada za Serikali za kuimarisha uwajibikaji, ufanisi na tija katika mashirika ya umma. Itatumika kufuatilia na kupima utekelezaji wa mikataba ya utendaji kazi ya Taasisi na Mashirika ya Umma, sambamba na kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali za Taifa.



***(Afisa Mitaji ya Umma Ndugu Abdullah Salum Abdullah akitoa ufafanuzi wa jinsi ya upigaji wa hesabu katika Nyenzo ya kufanya ufuatiliaji wa Mashirika ya Uwekezaji wa Umma)***

Uandaaji wa nyenzo hizi (ni hatua kubwa katika kuhakikisha Mashirika ya Uwekezaji wa Umma yanafanya kazi kwa uwajibikaji, kwa kuzingatia dira ya kitaifa na kuleta thamani ya fedha (value for money). Nyenzo hii itarahisisha kufuatilia mwenendo wa mashirika, kubaini mapungufu, na kuchukua hatua za haraka katika kutatua changamoto zinazojitokeza.

# OFISI YA MSAJILI WA HAZINA YAFUNGA MIKATABA YA KIUTENDAJI (PERFORMANCE CONTRACT) NA MASHIRIKA 9 YA UMMA KWA AWAMU YA PILI

KIKAO hicho kilifanyika siku ya Jumanne ya tarehe 16 Septemba 2025 katika ukumbi wa ZURA Zanzibar. Walioshiriki katika kikao hicho ni Wenyeviti wa Bodi za Mashirika ya Umma, Wakuu wa Mashirika ya Umma, Maafisa kutoka Mashirika ya Umma na Maafisa kutoka Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Kikao hiki kiliandaliwa kwa mujibu wa kifungu cha 35(i) cha Sheria ya Ofisi ya Msajili wa Hazin ana Usimamzi wa Mali za Umma nambari 6 ya mwaka 2021, na kilihudumiwa na Wenyeviti wa Bodi za Mashirika ya Umma, Wakuu wa Mashirika pamoja na maafisa kutoka Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Lengo kuu la kikao hicho ni kutoa mwelekeo wa utekelezaji wa mikataba hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na kuweza kuweka misingi ya uwajibikaji kwa mashirika ya umma kwa ulipaji wa gawio kwa Serikali pamoja na kutoa huduma iliyo bora kwa jamii.

Ufungaji huo wa Mikataba ya utendaji baina ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na wenyeviti wa mashirika tisa (09) ya uwekezaji wa Umma ni Pamoja na Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC), Shirika la Meli Zanzibar (SHIPCO), Shirika la Magazeti ya Serikali (CGN), Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), Shirika la Taifa la Biashara Zanzibar (ZSTC), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF), Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Mfuko wa Huduma za Afya (ZHSF) na Shirika la Bima Zanzibar (ZIC).

Kupitia zoezi hili la kusaini mikataba ya kiutendaji kwa mashirika tisa ya Serikali, Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar imeimarisha msingi wa uwajibikaji, uwazi na ufanisi katika utendaji wa mashirika ya umma na kutekeleza matakwa ya Sheria. Hatua hii inalenga kuhakikisha mashirika ya umma yanafanya kazi kwa weledi, yanatoa huduma bora kwa jamii na yanachangia ipasavyo katika ukuaji wa uchumi wa Taifa. Matukio ya Ufungaji wa Mikatab ani kama invyoonekana hapo chini



*Msajili Wa Hazina akitoa maelezo juu ya mikataba ya utendaji kazi.*




*Msajili wa Hazina Zanzibar Ndugu Waheed Muhammad Ibrahim Sanya (aliyekaa kulia) asaini Mkataba wa utendaji na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Taifa la Biashara Zanzibar ZSTC Bi. Kidawa Hamid Saleh (aliyekaa kushoto)*.

*Msajili wa Hazina Zanzibar Ndugu Waheed Muhammad Ibrahim Sanya (aliyekaa kulia) asaini Mkataba wa utendaji naMwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC) Bw. Ali Mzee Ali. (aliyekaa kushoto).*






*Msajili wa Hazina Zanzibar Ndugu Waheed Muhammad Ibrahim Sanya (aliyekaa kulia) asaini Mkataba wa utendaji na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Utangazaji (ZBC) Dk. idrissa Muslim Hija (aliyekaa kushoto).*



*Msajili wa Hazina Zanzibar Ndugu Waheed Muhammad Ibrahim Sanya (aliyekaa kulia) asaini Mkataba wa Kiutendaji na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Bandari Zanzibar Ndugu. Ndugu Joseph Abdalla Meza (aliyekaa kushoto)*



*Msajili wa Hazina Zanzibar Ndugu Waheed Muhammad Ibrahim Sanya (aliyekaa kulia) asaini Mkataba wa Kiutendaji na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Meli Zanzibar Ndugu. CDR Mohammed Khamis Makame (aliyekaa kushoto)*



*Msajili wa Hazina Zanzibar Ndugu Waheed Muhammad Ibrahim Sanya (aliyekaa kulia) asaini Mkataba wa Kiutendaji na Makamo Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar Ndugu. Mwantum Khamis Othman (aliyekaa kushoto)*

Aidha baada ya kukamilika kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Ofisi ya Msajili wa Hazina itafanya Tathmini ya Utendaji kwa kushirikiana na Mashirika hayo na kuiwasilisha kwa Mashirika hayo kwa hatua za uimarishaji.



*(Msajili wa Hazina Zanzibar Ndugu Waheed Muhammad Ibrahim Sanya (aliyekaa kulia) asaini Mkataba wa Kiutendaji na Makamo Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Magezeti ya Serikali Zanzibar Ndugu. Salum Juma Ali (aliyekaa kushoto).*



*Msajili wa Hazina Zanzibar Ndugu Waheed Muhammad Ibrahim Sanya (aliyekaa kulia) asaini Mkataba wa Ulipaji wa Gawio na Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), Dkt. Huda Ahmed Yussuf (aliyekaa kushoto).*

# OFISI YA MSAJILI WA HAZINA YAWASILISHA RIPOTI YA TATHMINI YA MKATABA WA KIUTENDAJI KWA WENYEVITI WA BODI, WATENDAJI WAKUU WA MASHIRIKA YA UMMA NA WAANDISHI WA HABARI

*Mkurugenzi wa Idara ya Mitaji ya Umma na Uwekezaji Ofisi ya Msajili wa Hazina Ndugu Ramia Mohammed Ramia awasilisha Ripoti ya Tathmini ya Mikataba ya Kiutendaji ya mwaka 2024/2025)*



OFISI ya Msajili wa Hazina Zanzibar imeendelea na utekelezaji wa jukumu lake la kusimamia utendaji wa mashirika ya umma kwa kufuata sheria na misingi ya uwajibikaji. Katika hatua hii, Ofisi imekagua na kutoa tathmini ya mikataba ya kiutendaji ya mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Akiwasilisha ripoti ya tathmini ya Mikataba wa utendaji kwa niaba ya Msajili wa Hazina Mkurugenzi wa Idara ya Mitaji ya Umma na Uwekezaji Ndugu Ramia Mohammed Ramia alisema yafuatayo:

Lengo la tathmini hii ni kubaini kiwango cha utekelezaji wa mikataba ya kiutendaji, kusisitiza uwajibikaji wa mashirika ya umma, na kutoa mwelekeo wa maboresho ili kuongeza ufanisi na huduma bora kwa jamii.

Tathmini hiyo ilionyesha ufanisi na changamoto zilizokabili mashirika katika utekelezaji wa wajibu wao ambapo Wenyeviti wa Bodi na Wakuu wa Mashirika walipokea ripoti hiyo, na kupata mwongozo wa kuboresha utendaji na kuimarisha nidhamu ya kifedha.

Ripoti hii ya tathmini inathibitisha kwamba Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar imeweka msingi thabiti wa kuboresha utendaji wa mashirika ya umma, kuongeza uwajibikaji, na kuhakikisha huduma bora kwa wananchi. Hatua hii inalenga kuimarisha ufanisi, uwazi na mchango wa mashirika ya umma katika maendeleo ya Taifa.

Tathmini ya Mikataba ya Kiutendaji kwa Mashirika Umma Zanzibar iliyofanywa na Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar imehusisha Mashirika kumi (10) yakiwemo Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC), Shirika la Meli Zanzibar (SHIPCO), Shirika la Magazeti ya Serikali (CGN), Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), Shirika la Taifa la Biashara Zanzibar (ZSTC), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF), Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA), Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia (ZPDC) na Shirika la Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA).

Mashirika yalipimwa kwa kutumia vigezo vitano vikuu navyo ni : Usimamizi wa Rasilimali Watu (People Management), Utawala Bora na Udhibiti (Good Governance and Control), Huduma kwa Wateja (Customer Service), Utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Taasisi (Core Functions of Institution Mandates) na Usimamizi wa Kifedha (Financial Stewardship) ambapo kwa ujumla tathmini hii imeonekana kwamba Utawala Bora na Udhibiti ulipata kiwango cha juu zaidi 84.7%, ilifuatiwa na

Utekelezaji wa Majukumu ya Msingi ya taasisi kwa kupata 74.8% na Huduma kwa Wateja ilipata 73.6%. Changamoto kubwa zilionekana kwenye Usimamizi wa Rasilimali Watu 68.08% na Usimamizi wa Kifedha 67.36%.

Tathmini ilishauri kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi wa ndani na wa kisheria ili kuimarisha usimamizi wa kifedha, kutoa mrejesho wa mara kwa mara kwa wafanyakazi ili kuboresha utendaji, kuweka kumbukumbu sahihi za masuala ya wafanyakazi na wateja kwa lengo la kuongeza ufanisi, kuanzisha mipango ya dharura (Business Continuity Plan) ili kuhakikisha huduma muhimu zinaendelea hata wakati wa changamoto, kuweka malengo sahihi na ya kupimika hususan kwenye viashiria vya kifedha, na Kuweka mifumo ya motisha na adhabu ili kuongeza uwajibikaji na ufanisi wa kazi.

Tathmini hii imeonyesha kwamba mashirika ya umma Zanzibar yamepiga hatua katika maeneo ya utawala bora na utekelezaji wa majukumu ya msingi, lakini yanahitaji kufanya maboresho makubwa kwenye usimamizi wa rasilimali watu na fedha.

Kwa kuzingatia matokeo ya tathmini iliyofanyika, Ofisi ya Msajili wa Hazina imependekeza hatua zifuatazo kuchukuliwa na taasisi zote za Uwekezaji wa Umma zifanye tathmini ya vihatarishi na kuandaa rejesta ya hatari ili kusimamia changamoto zinazoweza kuathiri huduma, Kuanzishwa na kusimamiwa kwa mpango wa mwendelezo wa kazi ili kuhakikisha huduma muhimu haziathiriki endapo changamoto zitajitokeza na Kufanyika kwa ukaguzi wa ndani kwa wakati na utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi ili kuimarisha uwajibikaji wa kifedha. kutolewe mrejesho wa utendaji kazi kwa wafanyakazi mara kwa mara kwa lengo la kudhibiti utendaji kazi wa wafanyakazi, kukusanya na kuandika (kuweka rekodi) ya malalamiko ya wafanyakazi, maelezo ya mafunzo, malalamiko ya wateja na masuala yanayohusiana ili kuboresha ustawi wa wafanyakazi na wateja.

Kupitia ufungaji wa mikataba ya mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imeweka mkazo wa uwajibikaji, ufanisi na uwazi, ili kuhakikisha mashirika ya umma yanaendelea kuwa nguzo ya maendeleo ya uchumi na ustawi wa wananchi.



*Msajili wa Hazina Zanzibar Ndugu Waheed Muhammad Ibrahim Sanya katika picha ya Pamoja na baadhi ya wanakamati ya Uandaji wa Tathmini ya Mkataba wa Utendaji wa Mashirika ya Umma.*

# KWA MARA YA KWANZA MIKATABA YA ULIPAJI WA GAWIO YAFUNGWA KWA MASHIRIKA 4 ZANZIBAR

OFISI ya Msajili wa Hazina Zanzibar imeendeleza jitihada zake za kuhakikisha mashirika ya umma yanachangia mapato ya Serikali kwa kuzingatia sheria, miongozo, uwajibikaji na utawala bora. Hatua hii imeimarishwa kupitia kikao cha ufungaji wa mikataba ya ulipaji gawio, kilichofanyika tarehe 16 Septemba 2025 katika ukumbi wa ZURA, Zanzibar.

Lengo la kikao hiki lilikuwa ni kutoa mwelekeo na kutia saini mikataba ya ulipaji gawio kwa mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha 2025/2026, sambamba na kuweka msingi wa uwajibikaji na ufanisi wa kifedha ambapo Mashirika ya ZIC, ZPC, SHIPCO na ZSTC yalifunga mikataba ya makubaliano ya ulipaji wa Gawio ambapo wenyeviti wa Bodi walikubali na kuthibitisha utekelezaji wa mikataba hii kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina, Pia Msajili wa Hazina alisisitiza umuhimu wa mashirika ya umma kuchangia mapato ya Serikali kupitia gawio na kutoa huduma bora kwa Taifa na jamii kwa ujumla.

Kupitia zoezi hili la kusaini mikataba ya ulipaji gawio, Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar imeweka msingi thabiti wa uwajibikaji wa kifedha, nidhamu na mchango wa mashirika ya umma katika kukuza uchumi wa Taifa. Hatua hii inalenga kuhakikisha kwamba mashirika ya umma yanachangia mapato kwa wakati na kwa uwazi, huku yakitoa huduma bora kwa wananchi.




***Msajili wa Hazina Zanzibar Ndugu Waheed Muhammad Ibrahim Sanya (aliyekaa kulia) asaini Mkataba wa Ulipaji wa Gawio na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Bandari Zanzibar Ndugu. Joseph Abdalla Meza (aliyekaa kushoto).***




*Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar Dkt. Juma Malik Akil (aliyekaa katikati) ahudhuria kikao cha Utiaji wa Saini wa Mikataba ya Kiutendaji, mikataba ya Malipo ya Gawio Pamoja na ripoti ya Tathmini ya Mkataba wa Utendaji wa Mashirika ya Umma).*



*Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar Dkt. Juma Malik Akil (aliyekaa katika) ahudhuria kikao cha Utiaji wa Saini wa Mikataba ya Kiutendaji, mikataba ya Malipo ya Gawio Pamoja na ripoti ya Tathmini ya Mkataba wa Utendaji wa Mashirika ya Umma.*

# JICHO LA HAZINA

TOLEO NAMBA 008
SEPTEMBA, 2025

***Jicho la Hazina litaendelea kuangaza, kufuatilia na kuhakikisha Mashirika ya umma yanakuwa chachu ya maendeleo ya kiuchumi kwa Zanzibar na wananchi wake***



Msajili Wa Hazina Zanzibar https://trosmz.go.tz/ info@trosmz.go.tz

**MASHIRIKA YA UMMA IMARA, TAIFA IMARA, SHIRIKI KATIKA UCHAGUZI KWA SALAMA NA AMANI**